TBARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WANAFUNZI KATIKA UPIMAJI WA KITAIFA WA DARASA LA NNE (SFNA) 2015

# 03 MAARIFA YA JAMII

**BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA**

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WANAFUNZI KATIKA UPIMAJI WA KITAIFA WA DARASA LA NNE MWAKA 2015

# 03 MAARIFA YA JAMII

*Kimechapishwa na*

Baraza la Mitihani la Tanzania,
S.L.P. 2624,
Dar es Salaam, Tanzania.

**© Baraza la Mitihani la Tanzania, 2016**

Haki zote zimehifadhiwa.

## YALIYOMO


DIBAJI ..... iv

1.0 UTANGULIZI ..... 1

2.0 UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WANAFUNZI ..... 2

2.1 Sehemu A: Historia ..... 2

2.2 Sehemu B: Uraia ..... 10

2.3 Sehemu C: Jiografia ..... 17

3.0 UFAULU WA WANAFUNZI KWA KILA MADA ..... 32

4.0 HITIMISHO ..... 33

5.0 MAPENDEKEZO ..... 33

Kiambatisho A ..... 35

Kiambatisho B ..... 37

# DIBAJI

Taarifa ya Uchambuzi wa Majibu ya Maswali ya Upimaji wa Kitaifa wa Darasa la Nne katika somo la Maarifa ya Jamii mwaka 2015 imeandaliwa kwa lengo la kutoa mrejesho kwa wanafunzi, walimu, watunga sera, wakuza mitaala na wadau wengine wa elimu kuhusu namna wanafunzi walivyojibu maswali ya upimaji huu. Majibu ya wanafunzi ni kiashiria kimojawapo kinachoonesha mambo ambayo wanafunzi waliweza kujifunza kwa ufasaha na yale ambayo hawakuweza kujifunza kwa ufasaha katika kipindi cha miaka minne ya Elimu ya Msingi.

Katika taarifa hii, uchambuzi unaonesha kuwa mambo yafuatayo yamechangia baadhi ya wanafunzi kushindwa kujibu maswali ya mtihani kwa usahihi: Kushindwa kutambua matakwa ya swali; kuwa na uelewa mdogo wa mada mbalimbali; kutokuwa na ufahamu kabisa wa baadhi ya mada; kushindwa kuoanisha mada husika na maisha yao ya kila siku na kuchagua jibu zaidi ya moja kinyume na maelekezo katika upimaji. Aidha, wanafunzi waliokuwa na ufaulu mzuri walikuwa na maarifa juu ya mada mbalimbali hivyo waliweza kubaini matakwa ya maswali. Uchambuzi wa kila swali umefanyika ambapo dosari zilizojitokeza wakati wanafunzi walipokuwa wanajibu maswali zimeainishwa. Aidha, mada zilizokuwa na ufaulu mzuri, wastani na hafifu katika upimaji huu zimeainishwa.

Baraza la Mitihani la Tanzania lina imani kuwa mrejesho huu utawawezesha wadau mbalimbali wa elimu kuchukua hatua madhubuti ili kuboresha ufundishaji na ujifunzaji. Aidha, Baraza la Mitihani la Tanzania linaamini kuwa endapo taarifa hii itafanyiwa

kazi ipasavyo, itawezesha kuboresha kiwango cha ufaulu katika Upimaji wa Kitaifa wa Darasa la Nne kwa miaka ijayo.

Mwisho, Baraza la Mitihani linapenda kutoa shukurani za dhati kwa Maafisa Mitihani na wote waliohusika katika kuandaa taarifa hii. Baraza litashukuru kupokea maoni na mapendekezo kutoka kwa walimu, wanafunzi na wadau wengine wa elimu ambayo yatasaidia katika kuboresha Upimaji wa Kitaifa wa Darasa la Nne kwa miaka ijayo.



**Dkt. Charles E. Msonde**
**KATIBU MTENDAJI**

## 1.0 UTANGULIZI

Upimaji wa Kitaifa wa Darasa la Nne kwa somo la Maarifa ya Jamii ulifanyika tarehe 25 mwezi Novemba mwaka 2015. Jumla ya wanafunzi **1,076,086** walisajiliwa kufanya Upimaji ambapo wanafunzi **1,010,813** ndio waliofanya maswali ya Upimaji huu katika somo la Maarifa ya Jamii. Aidha, uchambuzi wa majibu ya Upimaji wa Kitaifa wa Darasa la Nne katika somo la Maarifa ya Jamii unaonesha kuwa wanafunzi **873,823 (86.4%)** ndio waliofaulu upimaji huo na wanafunzi **136,990 (13.6%)** walishindwa.

Maswali ya Upimaji wa Kitaifa wa Darasa la Nne kwa somo la Maarifa ya Jamii kwa mwaka 2015 yalikuwa 25 na yaligawanywa katika sehemu kuu tatu: Sehemu A: Historia, Sehemu B: Uraia, na Sehemu C: Jiografia. Wanafunzi walitakiwa kujibu maswali yote katika sehemu zote tatu. Aidha, walielekezwa kuchagua jibu/herufi sahihi na kuliandika/kuiandika katika nafasi iliyotolewa, kutafsiri/ kusoma ramani na alama pia kuoanisha fungu A na B. Majibu ya wanafunzi yamefanyiwa uchambuzi kwa kubainisha idadi ya wanafunzi waliojibu swali husika, chaguzi walizofanya na sababu zinazoweza kuwa zilichangia kuwafanya wachague/wasichague jibu sahihi. Hata hivyo, Makundi ya ufaulu wa wanafunzi yameoneshwa kwa kutumia rangi, ambapo rangi ya kijani inaonesha wanafunzi wenye ufaulu mzuri, njano inaonesha wanafunzi wenye ufaulu wa wastani na nyekundu inaonesha wanafunzi wenye ufaulu hafifu.

Taarifa hii imegawanywa katika sehemu tatu. Sehemu ya kwanza inahusu uchambuzi wa majibu ya somo la Historia, sehemu ya pili inaonesha uchambuzi wa majibu ya somo la Uraia na sehemu ya tatu inaonesha uchambuzi wa majibu ya somo la Jiografia.

## 2.0 UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WANAFUNZI

Uchambuzi wa majibu ya wanafunzi unaonesha kuwa jumla ya wanafunzi **1,010,813** (**93.9%)** walifanya maswali yote (1 - 25) ya Upimaji wa somo la Maarifa ya Jamii. Ufuatao ni uchambuzi wa majibu ya wanafunzi kwa kila swali katika sehemu zote tatu.

### 2.1 Sehemu A: Historia

**Swali la 1:** Familia hujumuisha

A watu wanaoishi kijiji kimoja

B watu wanaoishi mtaa mmoja


C baba, mama na watoto

D baba, mama na majirani.

Swali hili lilipima uwezo wa wanafunzi kubaini watu wanaounda familia. Wanafunzi wengi (81.8%) waliweza kubaini jibu sahihi C “baba, mama na watoto” pengine kutokana na ukweli kwamba wao pia ni sehemu ya familia hivyo ilikuwa rahisi kwao kufahamu kuwa baba na mama ni sehemu ya familia zao.

Jumla ya wanafunzi 184,293 (18.2%) walikosa swali hili. Wanafunzi waliochagua kipotoshi A “watu wanaoishi kijiji kimoja” na B “watu wanaoishi mtaa mmoja” pengine walivutiwa na dhana ya "umoja" inayojitokeza katika vipotoshi hivyo kwani wengi wanahusianisha familia na umoja. Aidha, yawezekana wanafunzi waliochagua kipotoshi D “baba, mama na majirani” walielewa kuwa pengine majirani ni sehemu ya familia kwa kuwa

hushirikiana na wanafamilia wote katika shughuli zote za kila siku hivyo kuwafanya wanafunzi hawa kutowatofautisha na wanafamilia wengine. Kwa ujumla yawezekana wanafunzi hawa walichagua vipotoshi hivyo kutokana na kuhusisha familia na mazingira halisi wanayotoka hivyo kuona watu wote kama familia moja. **Kielelezo 2.1.1** kinaonesha asilimia ya wanafunzi katika kila alama.




**Kielelezo 2.1.1** kinaonesha kuwa wanafunzi wengi waliweza kuchagua jibu sahihi. Aidha, wachache sana (0.01%) hawakujibu swali hili.

**Swali la 2:** Kati ya hatua zifuatazo, hatua ya mwisho ya mabadiliko ya binadamu kwa mujibu wa nadharia ya kisayansi ilikuwa

A Chimpanzii

B Homo habilisi


C Zinjanthropasi

D Homo Sapiensi.

Swali hili lilipima uwezo wa wanafunzi kubaini chimbuko la binadamu na mabadiliko yake kimaumbile katika zama mbalimbali kwa kutumia nadharia ya sayansi. Jumla ya wanafunzi 671,041 (66.4%) walikosa swali hili kwa kuchagua na kuandika vipotoshi A “chimpanzii”, B “Homo habilisi” na C “zinjanthropasi”. Wanafunzi hawa walikuwa na

mtazamo wa kisayansi unaoamini kuwa binadamu alitokana na maendeleo ya viumbe jamii ya nyani na alipita katika hatua mbalimbali lakini walishindwa kubaini hatua hizo kwa mtiririko sahihi.

Aidha, wanafunzi wachache (33.6%) walifanikiwa kuchagua na kuandika herufi ya jibu sahihi D "Homosapiensi". Wanafunzi hawa walikuwa na uelewa juu ya mtiririko sahihi wa hatua za kisayansi za maendeleo ya binadamu. **Kielelezo 2.1.2** kinaonesha asilimia ya wanafunzi katika kila alama.




**Kielelezo 2.1.2** kinaonesha kuwa zaidi ya nusu ya wanafunzi walishindwa kuchagua jibu sahihi na asilimia 0.02 hawakujibu.

**Swali la 3:** Binadamu alianza kufuga wanyama na ndege katika

A Zama za Mwisho za Mawe

B Zama za Chuma


C Zama za Kati za Mawe

D Zama za Mwanzo za Mawe.

Swali lililenga kupima uelewa wa wanafunzi kuhusu hatua mbalimbali za maendeleo ya kiuchumi na kijamii alizopitia binadamu katika Zama mbalimbali. Ufaulu katika swali hili ulikuwa hafifu kwani ni wanafunzi 335,377 (33.2%) tu

walipata swali hili kwa kuchagua na kuandika herufi ya jibu sahihi A “Zama za Mwisho za Mawe”. Wanafunzi hawa walikuwa na uelewa juu ya maendeleo ya binadamu kwa kila kipindi hivyo ilikuwa rahisi kwao kubaini jibu sahihi.

Aidha, jumla ya wanafunzi 675,198 (66.8%) walikosa swali hili. Katika kundi hili, wanafunzi wengi walivutiwa na kipotoshi B “Zama za Chuma” pengine kutokana na umuhimu wa chuma katika shughuli mbalimbali za kiuchumi hususan uwindaji ambao unashabihiana na shughuli za ufugaji. Aidha, wanafunzi waliochagua vipotoshi C “Zama za Kati za Mawe” na D “Zama za Mwanzo za Mawe” inawezekana walikuwa na uelewa kuwa binadamu alianza kufuga wanyama na ndege katika zama za mawe lakini hawakuwa na uelewa wa zama halisi za mawe ambazo ufugaji huo ulianza. **Kielelezo 2.1.3** kinaonesha asilimia ya wanafunzi katika kila alama.




**Kielelezo 2.1.3** kinaonesha kuwa wanafunzi wengi (66.80%) walishindwa kuchagua jibu sahihi na wachache (0.02%) hawakujibu.

**Swali la 4:** Mojawapo ya mila na desturi mbaya za Watanzania hapo zamani ni pamoja na

A jando na unyago


B utii wa sheria

C kuolewa na kuoa katika umri mdogo

D ulipaji wa mahari.

Swali hili lilipima uwezo wa wanafunzi kutathmini mila na desturi za zamani. Jumla ya wanafunzi 524,521 (51.9%) walichagua na kuandika herufi ya jibu sahihi C "kuolewa na kuoa katika umri mdogo". Licha ya kufundishwa shuleni, wanafunzi hawa pengine waliweza kubaini jibu sahihi kwa sababu walikuwa na uelewa juu ya athari mbalimbali zitokanazo na ndoa za utotoni katika jamii zao.

Aidha, jumla ya wanafunzi 486,109 (48.1%) walishindwa swali hili. Wanafunzi waliochagua kipotoshi A "jando na unyago" yawezekana walikuwa na uelewa juu ya baadhi ya matendo yasiyofaa yafanyikayo katika jamii wakati wa jando na unyago kama vile ukeketaji wa wanawake kwa baadhi ya jamii lakini wakashindwa kufahamu kuwa kwa ujumla jando na unyago huwa na mafunzo yenye manufaa kwa ajili ya kuwandaa vijana kukabiliana na changamoto mbalimbali katika jamii. Wanafunzi waliochagua kipotoshi B "utii wa sheria" walishindwa kuelewa kuwa utii wa sheria hauhusiani na mila na desturi mbaya na wanafunzi waliochagua kipotoshi D "ulipaji wa mahari" walikosa ujuzi na maarifa ya kutathmini mila na desturi za Kitanzania kwani ulipaji wa mahari ni moja ya mila na desturi nzuri miongoni mwa makabila mengi ya Kitanzania. **Kielelezo 2.1.4** kinaonesha asilimia ya wanafunzi katika kila alama kwenye swali hili.





**Kielelezo 2.1.4** kinaonesha kuwa zaidi ya nusu ya wanafunzi waliweza kuchagua herufi ya jibu sahihi. Aidha, asilimia 0.02 hawakujibu.

**Swali la 5**: Muungano wa familia nyingi zenye asili moja hutengeneza____________________. (Ukoo, kabila, jamii, taifa)

Swali lililenga kupima uwezo wa wanafunzi katika kutambua chimbuko la ukoo. Swali hili lilitarajiwa kuwa na ufaulu mzuri ikizingatiwa kuwa kila mwanafunzi anatoka katika mojawapo ya koo zilizopo nchini. Jumla ya wanafunzi 664,628 (65.8%) waliweza kuchagua na kuandika jibu sahihi "ukoo". Wanafunzi hawa walitambua kuwa ukoo ni muunganiko wa familia nyingi zenye uhusiano wa damu.

Hata hivyo, jumla ya wanafunzi 345,030 (34.1%) waliochagua vipotoshi "kabila", "jamii" na "taifa" walishindwa kutambua mahusiano kati ya jamii, kabila na taifa kwani kabila hujumuisha watu wanaotoka katika eneo moja na kuongea lugha inayofanana; wakati jamii ni mkusanyiko wa watu wenye lengo moja; na taifa hujumuisha jamii mbalimbali katika nchi. **Kielelezo 2.1.5** kinaonesha asilimia ya wanafunzi katika kila alama.





**Kielelezo 2.1.5** kinaonesha kuwa wanafunzi wengi waliweza kuchagua na kuandika jibu sahihi “ukoo” na wachache sana (0.11%) hawakujibu.

**Swali la 6:** Wakati wa biashara ya kubadilishana bidhaa ________________. walikuwa na bidhaa za chuma. (Wayao, Wasukuma, Wavinza Wapare)

Swali hili lililenga kupima uelewa wa wanafunzi juu ya bidhaa mbalimbali zilizotumika kubadilishana na jamii za Tanzania zilizohusika. Swali hili ni miongoni mwa maswali yaliyokuwa na ufaulu hafifu kwani jumla ya wanafunzi 700,494 (69.3%) walishindwa kwa kuchagua na kuandika vipotoshi “Wayao”, “Wasukuma” na “Wavinza”. Wanafunzi hawa hawakuelewa kuwa makabila haya hayakuwa maarufu katika uzalishaji wa chuma.

Aidha, jumla ya wanafunzi 309,087 (30.6%) walikuwa na uelewa kuwa jamii za kale zilifanya biashara kwa kutumia rasimali zilizopatikana katika maeneo yao hivyo kuchagua na kuandika jibu sahihi “Wapare” ambao walikuwa maarufu katika ufuaji wa chuma. **Kielelezo 2.1.6** kinaonesha asilimia ya wanafunzi katika kila alama kwenye swali hili.





**Kielelezo 2.1.6** kinaonesha kuwa wanafunzi wengi walishindwa kuchagua na kuandika jibu sahihi na wachache sana (0.12%) hawakujibu.

**Swali la 7:** Mfumo wa kwanza wa uzalishaji mali usio wa kinyonyaji ambao jamii za Kitanzania zimepitia uliitwa_____________. (ujamaa, ubepari, utumwa, ujima)

Swali lilipima uelewa wa wanafunzi juu ya mifumo mbalimbali ya uzalishaji aliyopitia binadamu. Jumla ya wanafunzi 543,371 (53.8%) walishindwa swali hili. Wanafunzi waliochagua na kuandika kipotoshi "ujamaa" walishindwa kubaini kuwa japo mfumo huu haukuwa wa kinyonyaji lakini haukuwa wa kwanza. Aidha, waliochagua vipotoshi "ubepari" na "utumwa" walishindwa kuelewa kuwa mifumo hii ilikuwa ya kinyonyaji.

Hata hivyo, wanafunzi 463,273 (45.8%) waliweza kuchagua na kuandika jibu sahihi "ujima" ambao ndio mfumo wa kwanza wa uzalishaji mali ambao haukuwa wa kinyonyaji. **Kielelezo 2.1.7** kinaonesha asilimia ya wanafunzi katika kila alama.




**Kielelezo 2.1.7** kinaonesha kwamba swali hili lilikuwa na ufaulu wa wastani kwani wanafunzi asilimia 45.83 waliweza kuchagua na kuandika jibu sahihi.

## 2.2 Sehemu B: Uraia

**Swali la 8:** Mwanaume na mwanamke katika Nembo ya Taifa huwakilisha

A wafanyakazi

B wakulima


C umoja

D uhuru.

Swali lililenga kupima uwezo wa wanafunzi katika kutafsiri alama za Nembo ya Taifa. Swali hili lilikuwa na ufaulu wa wastani kwani jumla ya wanafunzi 472,893 (46.8%) tu waliweza kuchagua na kuandika herufi ya jibu sahihi C "umoja". Kimsingi alama hii uonesha ushirikiano uliopo katika Taifa kati ya wanaume na wanawake bila kujali jinsi.

Kwa upande mwingine, jumla ya wanafunzi 537,750 (53.2%) walivutiwa na vipotoshi A "wafanyakazi" na B "wakulima" pengine kutokana na ukweli kwamba, katika jamii yoyote wakulima na wafanyakazi ni wanaume na wanawake. Wanafunzi waliochagua kipotoshi D "uhuru" walishindwa kuelewa kuwa uhuru si mojawapo ya alama

iliyoko kwenye Nembo ya Taifa. **Kielelezo 2.2.1** kinaonesha asilimia ya wanafunzi katika kila alama.




**Kielelezo 2.2.1** kinaonesha kuwa zaidi ya nusu ya wanafunzi walishindwa kuchagua jibu sahihi na asilimia 0.02 hawakujibu swali hili.

**Swali la 9:** Muungano wa Tanganyika na Zanzibar huadhimishwa kila mwaka tarehe

A 12 Januari


B 26 Aprili

C 01 Mei

D 07 Julai.

Swali hili lilipima uwezo wa wanafunzi kubainisha sikukuu za kitaifa nchini Tanzania. Swali hili lilikuwa na ufaulu wa wastani kwani takriban nusu ya wanafunzi 514,669 (50.92%) walishindwa kwa kuchagua vipotoshi A “12 januari”, C “01 Mei” na D “07 Julai”. Wanafunzi hawa walivutiwa na umaarufu wa tarehe hizi kwani tarehe 12 Januari ni Sikukuu ya Mapinduzi ya Zanzibar, 01 Mei ni siku ya wafanyakazi Duniani na 07 Julai ni Siku ya Maonesho ya Biashara (Sabasaba) ambapo maonesho ya bidhaa mbalimbali huoneshwa kitaifa na kimataifa.

Hata hivyo, jumla ya wanafunzi 496,017 (49.07%) walifanikiwa kuchagua na kuandika jibu sahihi B “26 Aprili” tarehe ambayo Muungano huu ulirasimishwa. Hii inaonesha kuwa wanafunzi hawa walikuwa na maarifa ya kutosha juu ya dhana ya sikukuu za kitaifa hivyo kubaini sikukuu hii miongoni mwa sikukuu zilizotajwa. **Kielelezo 2.2.2** kinaonesha asilimia ya wanafunzi katika kila alama kwenye swali hili.




**Kielelezo 2.2.2** kinaonesha kwamba karibu nusu ya wanafunzi waliofanya swali hili waliweza kuchagua jibu sahihi “26 April” na wachache sana (0.01%) hawakujibu.

**Swali la 10:** Bendera ya Taifa ina rangi ngapi?

A Moja.

B Mbili.


C Tatu.

D Nne.

Swali lilipima uwezo wa wanafunzi kubaini idadi ya rangi katika Bendera ya Taifa ya Tanzania. Swali hili lilikuwa na ufaulu mzuri ambapo wanafunzi 803,761 (79.5%) waliweza kuchagua na kuandika herufi ya jibu sahihi D “Nne”. Licha ya kuwa hufundishwa darasani, kuwapo kwa Bendera ya Taifa katika shule na ofisi za serikali pengine huenda

kulichangia ufahamu wa wanafunzi kuhusu rangi za bendera ya Taifa.

Aidha, wanafunzi 206,941 (20.5%) waliochagua vipotoshi A "Moja", B "Mbili" na C "Tatu" hawakuwa na uelewa wa kutosha juu ya mada ya Alama za Taifa. **Kielelezo 2.2.3** kinaonesha asilimia ya wanafunzi katika kila alama.




**Kielelezo 2.2.3** kinaonesha kuwa wanafunzi wengi waliweza kuchagua herufi ya jibu sahihi na wachache sana (0.01%) hawakujibu.

**Swali la 11:** Mali ya familia inatakiwa kulindwa na

A watoto peke yao

B baba na mama


C kila mwanafamilia

D babu na bibi.

Swali lilipima uelewa wa wanafunzi juu ya ulinzi na usalama wa mali ya familia. Jumla ya wanafunzi 512,831 (50.7%) washindwa swali hili kwa kuchagua na kuandika vipotoshi A "Watoto peke yao" B "baba na mama" na D "babu na bibi".

Wanafunzi hawa walishindwa kujua kuwa jukumu la ulinzi na usalama ni la kila mtu katika familia.

Hata hivyo, jumla ya wanafunzi 497,860 (49.3%) waliweza kuchagua na kuandika jibu sahihi C “kila mwanafamilia”. Wanafunzi hawa walitambua kuwa kila mtu katika familia anao wajibu wa kulinda na kutunza mali ya familia. Yawezekana wanafunzi hawa walihawilisha maarifa ya kile kinachofanyika kwenye familia zao. **Kielelezo 2.2.4** kinaonesha asilimia ya wanafunzi katika kila alama.




**Kielelezo 2.2.4** kinaonesha kuwa swali hili lilikuwa na ufaulu wa wastani kwani karibu nusu ya wanafunzi (49.25%) waliweza kuchagua jibu sahihi.

**Swali la 12**: Kabla ya kuvuka barabara eneo lisilo na taa au alama za pundamilia unashauriwa kuangalia upande wa

A kulia, kushoto na kulia tena

B kushoto, kulia na kushoto tena


C kulia na kushoto tu

D kushoto na kulia tu.

Swali hili lilipima uelewa wa wanafunzi juu ya matumizi sahihi ya barabara. Swali hili lilikuwa na ufaulu wa wastani kwani ni wanafunzi 422,833 (41.8%) tu ndio waliweza

kuchagua na kuandika jibu sahihi A “kulia, kushoto na kulia tena”. Wanafunzi hawa huenda walitambua kuwa kabla ya kuvuka barabara, sharti uangalie upande wa kulia kwanza kisha kushoto na kuangalia kulia tena kwani wakati unaangalia kushoto huenda gari likatokea upande wa kulia.

Hata hivyo, jumla ya wanafunzi 587,801(58.2%) walishindwa swali hili. Wanafunzi waliochagua kipotoshi B “kushoto, kulia na kushoto tena” hawakuwa na ufahamu wa upande upi wa kwanza kuangalia kabla ya kuvuka barabara. Aidha, wanafunzi waliochagua vipotoshi C “Kulia na kushoto tu” na D “Kushoto na kulia tu” hawakuwa na maarifa ya namna nzuri ya kuvuka barabara kwani ni hatari kutofuata kanuni za barabarani. **Kielelezo 2.2.5** kinaonesha asilimia ya wanafunzi katika kila alama kwenye swali hili.





**Kielelezo 2.2.5** kinaonesha kuwa wanafunzi wengi walishindwa kuchagua herufi ya jibu sahihi na wachache sana (0.02%) hawakujibu.

**Swali la 13**. Faida mojawapo ya kuwashirikisha watoto katika maamuzi ni __________________. (kuwapeleka watoto shule, kuwasikiliza maoni yao, kuwapa watoto upendeleo)

Swali lilipima uelewa wa wanafunzi juu ya faida ya kuwashirikisha watoto katika maamuzi. Swali hili lilikuwa na ufaulu hafifu kwani jumla ya wanafunzi 735,068 (72.7%)

walichagua na kuandika vipotoshi “kuwapeleka watoto shule” na “kuwapa watoto upendeleo”. Wanafunzi hawa walishindwa kufahamu kuwa kuwapeleka watoto shule ni mojawapo ya haki za watoto wakati kuwapa watoto upendeleo huwafanya wasiwe na mwenendo mzuri.

Aidha, ni wanafunzi 273,857 (27.1%) tu walioweza kuchagua na kuandika jibu sahihi “kusikilizwa maoni yao” kwani watoto wakishirikishwa katika maamuzi maoni yao husikilizwa. **Kielelezo 2.2.6** kinaonesha asilimia ya wanafunzi katika kila alama.





**Kielelezo 2.2.6** kinaonesha kuwa wanafunzi wengi (72.72%) walishindwa kuchagua na kuandika jibu sahihi na wachache (0.19%) hawakujibu.

**Swali la 14**: Alama inayoonekana kwenye Bendera ya Rais ni ________________. (jembe na nyundo, Nembo ya Taifa, mwenge wa uhuru)

Swali lilipima uelewa wa wanafunzi juu ya alama iliyopo kwenye Bendera ya Rais. Swali hili lilikuwa na ufaulu hafifu kwani jumla ya wanafunzi 638,637 (63.2%) walichagua vipotoshi “jembe na nyundo” na “mwenge wa uhuru”. Wanafunzi hawa walivutiwa na vipotoshi hivi pengine kutokana na ukweli kwamba alama ya jembe na nyundo ni

maarufu kwa kuwa ipo kwenye bendera ya Chama cha Mapinduzi (CCM) ambayo huonekana maeneo wanayokaa baadhi ya wanafunzi na mwenge wa uhuru ambao hukimbizwa nchi nzima huwavutia watu wengi kutokana na kuhimiza umoja na mshikamano.

Aidha, ni wanafunzi 370,590 (36.7%) tu walichagua na kuandika jibu sahihi “Nembo ya Taifa”. Wanafunzi hawa walidhihirisha kuwa na ufahamu wa kutosha kuhusu “Alama za Taifa”. **Kielelezo 2.2.7** kinaonesha asilimia ya wanafunzi katika kila alama kwenye swali hili.




**Kielelezo 2.2.7** kinaonesha kwamba swali hili lilikuwa na ufaulu hafifu kwani asilimia 63.18 ya wanafunzi walishindwa kuchagua na kuandika jibu sahihi.

## 2.3 Sehemu C: Jiografia

**Swali la 15:** Vitu vyote vinavyomzunguka binadamu na viumbe wengine huitwa

A mbuga za wanyama


B mazingira

C bahari na misitu

D Ardhi na misitu.

Swali hili lilipima uelewa wa wanafunzi juu ya maana ya mazingira. Ufaulu katika swali hili ulikuwa mzuri kwani wanafunzi 692,660 (68.5%) waliweza kuchagua na kuandika herufi ya jibu sahihi B “Mazingira” kwani mazingira ni vitu vyote vinavyomzunguka binadamu na viumbe vingine.

Aidha, wanafunzi 317,913 (31.5%) waliochagua vipotoshi A “Mbuga za wanyama” C “bahari na misitu” na D “Ardhi na misitu” walishindwa kuelewa kuwa mbuga za wanyama, bahari, misitu na ardhi pia ni sehemu ya mazingira. **Kielelezo 2.3.1** kinaonesha asilimia ya wanafunzi katika kila alama kwenye swali hili.




**Kielelezo 2.3.1** kinaonesha kuwa wanafunzi wengi waliweza kuchagua herufi ya jibu sahihi na asilimia 0.02 tu hawakujibu.

**Swali la 16:** Pande kuu nne za dunia hutambuliwa kwa kutumia

A mawio na machweo ya jua


B picha na ramani

C ufunguo na kipimio

D mkono wa kushoto na kulia.

Swali lilipima ujuzi wa wanafunzi katika kubainisha pande kuu nne za dunia. Swali hili lilikuwa na ufaulu hafifu kwani jumla ya wanafunzi 733,920 (72.6.%) walishindwa kuchagua jibu sahihi. Wanafunzi hawa walichagua vipotoshi B “picha na ramani”, C “Ufunguo na kipimio” na D “mkono wa kushoto na kulia” ambavyo havina uhusiano katika utambuzi wa pande kuu za dunia.

Aidha, jumla ya wanafunzi 276,644 (27.38%) waliweza kuchagua jibu sahihi A “mawio na machweo ya jua”. Wanafunzi hawa walielewa kuwa jua huchomoza upande wa Mashariki na huchwa upande wa Magharibi. Hivyo, kwa kuelewa pande hizi, ilikuwa ni rahisi kwao kuelewa pande kuu nne za dunia. **Kielelezo 2.3.2** kinaonesha asilimia ya wanafunzi katika kila alama.




**Kielelezo 2.3.2** kinaonesha kwamba wanafunzi wengi walishindwa kuchagua jibu sahihi na wachache (0.02%) hawakujibu.

**Swali la 17**: Baadhi ya shughuli za kiuchumi nchini Tanzania ni pamoja na

A kilimo, siasa na ufugaji

B uvuvi, utalii na Sayansi


C viwanda, utalii na burudani

D kilimo, utalii na viwanda.

Swali hili lilipima ufahamu wa wanafunzi juu ya shughuli za kiuchumi nchini Tanzania. Swali hili lilikuwa na ufaulu hafifu kwani wanafunzi 713,053 (70.5%) walichagua na kuandika vipotoshi A “kilimo, siasa na ufugaji”, B “uvuvi, utalii na sayansi” na C “viwanda, biashara na burudani”. Wanafunzi hawa walishindwa kuelewa kuwa “siasa”, “sayansi na “burudani” si shughuli za kiuchumi. Pengine wanafunzi hawa walivutiwa na vipotoshi vyenye shughuli hizi kwa kuwa hufanyika mara kwa mara katika jamii wanazoishi.

Ni wanafunzi 297,502 (29.4) tu walioweza kuchagua na kuandika jibu sahihi D “kilimo, utalii na viwanda”. Wanafunzi

hawa waliweza kupata swali hili pengine kutokana na ukweli kwamba, shughuli za kilimo, utalii na viwanda hufanyika katika mazingira wanayoishi. Hivyo, licha ya kufundishwa shuleni, wanafunzi hawa waliweza kuhawilisha maarifa. **Kielelezo 2.3.3** kinaonesha asilimia ya wanafunzi katika kila alama kwenye swali hili.




**Kielelezo 2.3.3** kinaonesha kwamba swali hili lilikuwa na ufaulu hafifu kwani wanafunzi wengi (70.5%) walishindwa kuchagua herufi ya jibu sahihi.

**Swali la 18:** Mojawapo ya faida ya utalii nchini Tanzania ni

A kuleta mvua za msimu

B kukuza pato la taifa


C kufanya utafiti wa mazingira

D kuleta mazao ya biashara.

Swali hili liliwataka wanafunzi kubaini faida za utalii nchini Tanzania. Ufaulu katika swali hili ulikuwa wa wastani kwani ni wanafunzi 469,605 (46.5%) tu waliweza kuchagua na kuandika jibu sahihi B “kukuza pato la taifa”. Wanafunzi

hawa walikuwa na ufahamu juu ya mchango wa sekta ya utalii katika Taifa.

Aidha, jumla ya wanafunzi 540,972 (53.5%) waliochagua vipotoshi A "Kuleta mvua za msimu", C "kufanya utafiti wa mazingira" na D "kuleta mazao ya biashara" walishindwa kuelewa kuwa vipotoshi hivi havina uhusiano na msingi wa swali. Hivyo, ni dhahiri kuwa wanafunzi hawa walishindwa kubaini matakwa ya swali hivyo kuchagua vipotoshi kwa kubuni tu. **Kielelezo 2.3.4** kinaonesha asilimia ya wanafunzi katika kila alama.




**Kielelezo 2.3.4** kinaonesha kuwa zaidi ya nusu ya wanafunzi (53.52%) waliojibu swali hili walishindwa kuchagua jibu sahihi.

**Swali la 19:** Moja kati ya shughuli zifuatazo husababisha uharibifu wa mazingira kwa kiasi kikubwa

A upandaji miti

B ufugaji kuku kwa wingi


C ukataji miti ovyo

D kilimo cha mpunga.

Swali liliwataka wanafunzi kubaini shughuli za kiuchumi zinazoharibu mazingira kwa kiasi kikubwa. Swali hili lilikuwa na ufaulu mzuri kwani jumla ya wanafunzi 721,447 (71.4%) waliweza kuchagua na kuandika herufi ya jibu sahihi C

“ukataji miti ovyo”. Wanafunzi hawa pengine walihusianisha uharibifu wa mazingira katika maeneo yao na ukataji miti ovyo kwa ajili ya shughuli mbalimbali za kiuchumi na kijamii.

Wanafunzi hawa walionesha umahiri na uelewa mkubwa kwani vipotoshi vingine katika swali hili vilivyowavutia wanafunzi 289,080 (28.6.%) vina uhusiano kwa kiasi kidogo na jibu sahihi. “Ufugaji kuku kwa wingi” kwa mfano, huweza kupelekea mmomonyoko wa udongo na uchafuzi wa hali ya hewa. Vilevile “kilimo cha mpunga” kama hakitakuwa cha mfumo wa majaruba huweza kupunguza rutuba ya udongo. Aidha, wanafunzi waliochagua kipotoshi A “upandaji miti” walishindwa kuelewa kuwa upandaji miti huboresha mazingira. **Kielelezo 2.3.5** kinaonesha asilimia ya wanafunzi katika kila alama.




**Kielelezo 2.3.5** kinaonesha kuwa wanafunzi wengi waliweza kuchagua herufi ya jibu sahihi ilhali wanafunzi wachache sana (0.03%) hawakujibu swali hili.

Katika swali la 20 hadi 23 wanafunzi walitakiwa kubainisha vifaa vya kupimia hali ya hewa kutoka fungu B kwa kuoanisha na maswali kutoka fungu A kisha kuandika herufi ya jibu sahihi katika mabano.

**Majibu ya fungu A**

A Haigromita

B Kipima upepo

C Kipimajoto

D Baromita

E Kipima mvua


F Anemomita

G Kipimajua

**Swali la 20:** Kifaa kinachopima mwendokasi wa hewa iliyo katika mwendo

Swali liliwataka wanafunzi kubainisha kifaa kinachopima mwendo kasi wa hewa iliyo katika mwendo. Swali hili lilikuwa na ufaulu hafifu kwani jumla ya wanafunzi 838,436 (82.9%) walivutiwa na vipotoshi vilivyotolewa kwa kuwa vyote vinatumika kupima hali ya hewa. Aidha, kipotoshi B “Kipima upepo” kiliwavutia wanafunzi wengi zaidi kuliko vipotoshi vingine katika swali hili pengine kwa kuwa swali liliuliza juu ya kifaa cha kupima mwendo kasi wa hewa hivyo wanafunzi walihusianisha “upepo” na “hewa” iliyo katika mwendo.

Ni wanafunzi 171,368 (17%) tu walioweza kuchagua na kuandika herufi ya jibu sahihi F “Anemomita” ambacho ndicho kipimo kinachotumika kupima mwendo kasi wa hewa iliyo katika mwendo. **Kielelezo 2.3.6** kinaonesha asilimia ya wanafunzi katika kila jibu kwenye swali hili.





**Kielelezo 2.3.6** kinaonesha kwamba wanafunzi wengi walishindwa kuchagua na kuandika jibu sahihi na wachache sana (0.10%) hawakujibu swali hili.

**Swali la 21**: Kifaa kinachopima msukumo wa hewa

Swali hili liliwataka wanafunzi kubaini kifaa cha kupima msukumo wa hewa. Ufaulu katika swali hili pia ulikuwa hafifu kwani jumla ya wanafunzi 797,968 (78.9%) walivutiwa na vipotoshi na hasa kipotoshi F "Anemomita" kwa sababu walishindwa kutofautisha msukumo wa hewa na mwendokasi wa hewa.

Aidha, wanafunzi 211, 737 (20.9%) waliweza kuchagua na kuandika herufi ya jibu sahihi D "Baromita", ambacho ndicho kipimo kinachotumika kupima msukumo wa hewa. **Kielelezo 2.3.7** kinaonesha asilimia ya wanafunzi katika kila jibu.





**Kielelezo 2.3.7** kinaashiria kwamba swali hili lilikuwa na ufaulu mbaya kwani wanafunzi wengi (78.94%) walishindwa kuchagua herufi ya jibu sahihi.

**Swali la 22:** Kifaa kinachopima kiwango cha unyevu au mvuke wa maji yaliyo ndani ya hewa katika anga

Swali liliwataka wanafunzi kubainisha kifaa kinachotumika kupima unyevu au mvuke wa maji yaliyomo ndani ya hewa katika anga. Swali hili lilikuwa na ufaulu hafifu kwani wanafunzi walio wengi (80.7%) walishindwa kuchagua jibu sahihi. Wanafunzi hawa walishindwa kutofautisha kati ya hewa, upepo, unyevu na mvuke.

Hata hivyo, wanafunzi 193,648 (19.2%) waliweza kujibu swali hili kwa usahihi kwa kuchagua na kuandika herufi ya jibu sahihi A "Haigromita". **Kielelezo 2.3.8** kinaonesha asilimia ya wanafunzi katika kila alama kwenye swali hili.





**Kielelezo 2.3.8** kinaonesha kuwa swali hili lilikuwa na ufaulu hafifu kwani wanafunzi wengi (80.7%) walishindwa kuchagua na kuandika jibu sahihi na wachache (0.11%) hawakujibu.

**Swali la 23**: Kifaa kinanachopima hali ya joto au baridi ya kitu au mahali

Swali lililenga kupima uwezo wa wanafunzi wa kubainisha kifaa kinachopima hali ya joto au baridi ya kitu au mahali. Swali hili lilikuwa na ufaulu wa wastani kwani karibu nusu ya wanafunzi 483,856 (47.9%) waliweza kuchagua na kuandika herufi ya jibu sahihi C “kipimajoto”.


Hata hivyo, wanafunzi 525,852 (52%) walichagua vipotoshi, hali inayoonesha kuwa hawakuwa na ufahamu wa kutosha juu ya mada ya hali ya hewa. Aidha, wanafunzi wengi katika kundi hili walichagua kipotoshi G “kipimajua”. Pengine wanafunzi hawa walihusianisha jua na joto. **Kielelezo 2.3.9** kinaonesha asilimia ya wanafunzi katika kila alama.




**Kielelezo 2.3.9** kinaonesha kuwa swali hili lilikuwa na ufaulu wa wastani kwani karibu nusu ya wanafunzi (47.87%) waliweza kuchagua na kuandika jibu sahihi. Hata hivyo, asilimia 0.11 ya wanafunzi hawakujibu swali hili.

Katika swali la 24 na 25, wanafunzi walitakiwa kusoma mchoro wa alama na ramani kisha kujaza jibu sahihi.


**Swali la 24:** Alama hii hapa chini inawakilisha nini katika ramani? _______________.




Swali hili lilipima ujuzi wa wanafunzi kubaini alama mbalimbali ambazo hutumika katika ramani pamoja na kutambua matumizi yake. Swali lilikuwa na ufaulu hafifu zaidi likilinganishwa na maswali mengine katika somo la Maarifa ya Jamii kwani jumla ya wanafunzi 915,436 (90.6) walishindwa kuandika jibu sahihi. Wengi waliandika ufunguo, dira na pande kuu nne za dunia ambayo yote hayakuwa majibu sahihi kwa sababu ufunguo hutumika


kutafsiri alama mbalimbali zilizomo katika ramani ilhali dira ni kifaa kitumikacho kuonesha pande kuu nne za dunia.

kielelezo **2.3.10** kinaonesha sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyekosa swali hili.


24. Alama hii hapa chini inawakilisha nini katika ramani? Pande kuu za dunia.


**Kielelezo 2.3.10** kinaonesha mwanafunzi alijibu “pande kuu za dunia” ambalo halikuwa jibu sahihi.

Ni wanafunzi 91,106 (9%) tu walioweza kuandika jibu sahihi “uelekeo wa kaskazini”. Wanafunzi hawa walikuwa na uelewa wa kutosha juu ya maana ya ufunguo, dira, pande kuu nne za dunia na uelekeo wa kaskazini hivyo ilikuwa rahisi kwao kuandika jibu sahihi. **Kielelezo 2.3.11** kinaonesha asilimia ya wanafunzi katika kila alama kwenye swali hili.





**Kielelezo 2.3.11** kinaonesha kuwa swali hili lilikuwa na ufaulu hafifu kwani asilimia 90.58 ya wanafunzi walishindwa kuchagua na kuandika jibu sahihi na asilimia 0.40 hawakujibu.

**Swali la 25:** Usomaji wa ramani.

Swali lilipima uwezo wa wanafunzi kusoma ramani ya Tanzania na kubainisha maumbile mbalimbali yaliyopo kwenye sura ya nchi ambapo ramani ya Tanzania ilichorwa na wanafunzi walitakiwa kuandika jina la ziwa lililoandikwa herufi C.

Jumla ya wanafunzi 567,900 ( 56.2%) walikosa swali hili. Wanafunzi wengi katika kundi hili waliandika "Victoria" na "Nyasa". Wanafunzi hawa walionesha kutokuwa na ufahamu juu ya maziwa yaliyoko Tanzania. **Kielelezo 2.3.12** kinaonesha mfano wa mwanafunzi aliyekosa swali hili.


Soma ramani ifuatayo kisha jibu swali la 25.




25 Herufi **C** inawakilisha ziwa gani? Ziwa Viktoria.

Katika kielelezo **2.3.12**, mwanafunzi aliandika "ziwa Viktoria" ambalo siyo jibu sahihi.

Aidha, jumla ya wanafunzi 441,186 (43.6%) waliweza kuandika jibu sahihi "Tanganyika". Wanafunzi hawa walikuwa na ufahamu wa maziwa yaliyopo kwenye ramani ya Tanzania kwa ufasaha na hivyo kuandika jibu sahihi. **Kielelezo 2.3.13** kinaonesha asilimia ya wanafunzi katika kila alama.




**Kielelezo 2.3.13** kinaonesha kwamba zaidi ya nusu ya wanafunzi (56.18%) walishindwa kusoma ramani na kujaza jibu sahihi.

## 3.0 UFAULU WA WANAFUNZI KWA KILA MADA

Uchambuzi wa mada uliofanywa unaonesha kuwa baadhi ya mada zilikuwa na ufaulu mzuri na nyingine zilikuwa na ufaulu wa wastani na hafifu. Kwa ujumla, ufaulu wa wanafunzi katika mada ulikuwa wa wastani kwani mada 3 tu zilikuwa na ufaulu mzuri, mada 14 zilikuwa na ufaulu wa wastani na mada 1 ilikuwa na ufaulu hafifu. Aidha, ufaulu wa wanafunzi umeoneshwa katika Kiambatanisho A na B ambapo mada zilizokuwa na ufaulu hafifu zilikuwa na wastani wa ufaulu wa kati ya alama 0 hadi 21 (nyekundu), wastani 22 – 61 (njano) na ufaulu mzuri 62 – 100 (kijani).

Mada zilizokuwa na ufaulu mzuri ni “Familia Yetu”, “Ukoo Wetu” na “Mazingira”. Wanafunzi wengi walikuwa na uelewa wa kutosha katika mada hivyo kuweza kuchagua/kuandika jibu sahihi kutoka katika majibu waliyopewa.

Mada zingine kama vile “Utamaduni”, “Kukua kwa Mifumo ya Kiuchumi na Kiutawala katika Jamii za Tanzania hadi Karne ya 19”, “Alama za Taifa”, “Alama za Shule na Taifa”, “Ulinzi na Usalama katika Ngazi ya Familia”, “Ulinzi na Usalama katika Ngazi ya Shule” na “Vitu Vinavyounda Mazingira”, “Chimbuko na Mabadiliko ya Binadamu”, “Hatua za Maendeleo katika Zama Mbalimbali”, “Mahusiano Miongoni mwa Jamii za Kitanzania hadi Karne ya Kumi na Tisa”, “Misingi ya Demokrasia, “Ramani Rahisi”, “Shughuli za Kiuchumi katika Tarafa, Wilaya na Nchi” na “Hali ya

Hewa ya Tarafa, Wilaya na Nchi" zilikuwa na ufaulu wa wastani.

Mada pekee iliyokuwa na ufaulu hafifu ni "Uchoraji, Utengenezaji, Uundaji na Ujenzi wa Ramani".

## 4.0 HITIMISHO

Uchambuzi wa majibu ya maswali ya Upimaji wa Kitaifa wa Darasa la Nne katika somo la Maarifa ya Jamii unaonesha kuwa, kwa ujumla ufaulu wa wanafunzi katika somo hili ulikuwa mzuri kwani asilimia 86.4 ya wanafunzi walifaulu kwa kupata alama kati ya 11 hadi 50 na wanafunzi asilimia 13.6 walishindwa kwa kupata alama kati ya 0 hadi 10. Aidha, ufaulu wa jumla wa wanafunzi katika mada zote ulikuwa wa wastani.

## 5.0 MAPENDEKEZO

Ili kuboresha kiwango cha elimu na ufaulu kwa ujumla, Baraza la Mitihani linashauri yafuatayo:

(a) Walimu waweke mkazo katika kufundisha mada zote hususan mada ambazo wanafunzi hawakufanya vizuri.

(b) Wanafunzi wafundishwe namna ya kusoma maswali kwa umakini ili waweze kubaini matakwa ya kila swali kabla ya kuyajibu.

(c) Wanafunzi wahimizwe kusoma vitabu vingi vya kiada na ziada ili waweze kujiongezea maarifa.

(d) Walimu watunge maswali ya majaribio na mitihani ya mihula ambayo yatawapa ujuzi wanafunzi katika kujibu maswali yanayopima ujuzi mbalimbali

(e) Mamlaka zinazohusika na elimu zifuatilie changamoto mbalimbali zitokanazo na mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji.

*Kiambatisho A*

## UFAULU WA WANAFUNZI KATIKA KILA MADA

| Na | Mada | UPIMAJI WA 2015 | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | Ufaulu kwa kila Swali | | Wastani wa ufaulu (%) | Maoni |
| | | Namba ya Swali | % ya ufaulu | | |
| 1 | Familia Yetu | 1 | 81.8 | 81.8 | Mzuri |
| 2 | Mazingira | 15 | 64.4 | 67.9 | Mzuri |
| | | 19 | 71.4 | | |
| 3 | Ukoo Wetu | 5 | 65.8 | 65.8 | Mzuri |
| 4 | Alama za Shule na za Taifa | 10 | 79.5 | 58.1 | Wastani |
| | | 14 | 36.7 | | |
| 5 | Utamaduni | 4 | 51.9 | 51.9 | Wastani |
| 6 | Ulinzi na Usalama katika Ngazi ya Familia | 11 | 49.3 | 49.3 | Wastani |
| 7 | Alama za Taifa | 8 | 46.8 | 47.95 | Wastani |
| | | 9 | 49.1 | | |
| 8 | Kukua kwa Mifumo ya Kiuchumi na Kiutawala Katika Jamii za Tanzania Hadi Karne ya 19 | 7 | 45.8 | 45.8 | Wastani |
| 9 | Vitu Vinavyounda Mazingira | 25 | 43.6 | 43.6 | Wastani |
| 10 | Ulinzi na Usalama katika Ngazi ya Shule | 12 | 41.8 | 41.8 | Wastani |
| 11 | Shughuli za kiuchumi katika Tarafa, Wilaya na Nchi | 17 | 29.4 | 37.95 | Wastani |
| | | 18 | 46.5 | | |

| Na | Mada | UPIMAJI WA 2015 | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | Ufaulu kwa kila Swali | | Wastani wa ufaulu (%) | Maoni |
| | | Namba ya Swali | % ya ufaulu | | |
| 12 | Chimbuko na Mabadiliko ya Binadamu | 2 | 33.6 | 33.6 | Wastani |
| 13 | Hatua za Maendeleo katika Zama Mbalimbali | 3 | 33.2 | 33.2 | Wastani |
| 14 | Mahusiano Miongoni mwa Jamii za Kitanzania hadi Karne ya Kumi na Tisa | 6 | 30.6 | 30.6 | Wastani |
| 15 | Ramani Rahisi | 16 | 27.4 | 27.4 | Wastani |
| 14 | Misingi ya Demokrasia | 13 | 27.1 | 27.1 | Wastani |
| 17 | Hali ya hewa ya Tarafa, Wilaya na Nchi | 20 | 17.0 | 26.25 | Wastani |
| | | 21 | 20.9 | | |
| | | 22 | 19.2 | | |
| | | 23 | 47.9 | | |
| 18 | Uchoraji, Utengenezaji, Uundaji na Ujenzi wa Ramani | 24 | 9.0 | 9.0 | Hafifu |

*Kiambatisho B*

## UFAULU WA WANAFUNZI KATIKA KILA MADA

